JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

Mtaa wa Sheikhbad,
S.L.P. 1004,
65101LINDI,
Barua Pepe: rbclindi@pccb.go.tz.
TANZANIA.
www.pccb.go.tz

LINDI
Aprili 13, 2021

TAARIFA KWA UMMA

TAKUKURU MKOA WA LINDI YAOKOA SH. 139,260,169.00 NA KUWAFIKISHA WATUHUMIWA NANE (8) MAHAKAMANI KWA KUJIPATIA FEDHA ZAIDI YA SHILINGI MILIONI 150 KWA NJIA ZA UDANGANYIFU

Ndugu wanahabari,

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Lindi inajumuisha ofisi za TAKUKURU Lindi Mkoani, Kilwa, Nachingwea, Liwale na Ruangwa. Tumeendelea kutekeleza majukumu yetu katika robo ya tatu ya mwaka wa fedha 2020/2021 iliyoanzia Januari, 2021 hadi Machi, 2021, kama yanavyoainishwa katika Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Sura ya 329 Marejeo 2019. Majukumu yetu yalitekelezwa kupitia madawati mbalimbali ikiwemo Dawati la Uchunguzi, Huduma za Sheria na Mashitaka, Uzuiaji Rushwa pamoja na Elimu kwa Umma.

Ndugu wanahabari,

Kupitia dawati la uchunguzi, kwa kipindi cha Januari, 2021 hadi Machi, 2021 TAKUKURU Mkoa wa Lindi ilipokea jumla ya malalamiko 132 kuhusiana na vitendo vya rushwa na mambo mengine yanayoshabihiana na rushwa. Malalamiko haya yalihusu sekta mbalimbali zikiwemo: Elimu (7), Ardhi (11), Ushirika (70), Afya (4), Fedha (6), Jeshi la Polisi (1), Mahakama (3), Nishati (1), Tamisemi (2), Binafsi (12), Mawasiliano (1), Maendeleo ya jamii (4), Madini (1),

Biashara (3), Ujenzi (3), Utawala (4), Maji (1). Malalamiko haya yamefanyiwa kazi na yapo katika hatua mbalimbali na baadhi yake yamekamilika.

Ndugu wanahabari,

TAKUKURU Mkoa wa Lindi pia kwa kipindi tajwa imeokoa jumla ya kiasi cha **Shilingi 139,260,169.** Fedha zilizookolewa zilikuwa zimechepushwa na watu wachache kwa njia za udanganyifu na lengo la kujinufaisha, kinyume na Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11 ya Mwaka 2007. Fedha hizo zinajumuisha fedha za wakulima kwa mauzo ya korosho msimu wa 2020/2021 kiasi cha **shilingi 73,666,484.00** zilizotokana na udanganyifu mkubwa uliofanywa na Kampuni ya Mafubilo General Supplies Ltd kwa kushirikiana na Viongozi wa Vyama vya Msingi vya Ushirika (AMCOS) vya Ukombozi na Ndomondo vya NACHINGWEA. Baada ya kuanzisha uchunguzi, fedha zote zilirejeshwa Serikalini. Aidha kiasi cha **Shilingi 65,593,321.00** kilichobaki kilidhibitiwa na kurejeshwa kwa wahanga**.**

Ndugu wanahabari,

Kwa upande wa mashitaka, katika kipindi cha Januari 2021 hadi Machi 2021, TAKUKURU (M) Lindi ilifanikiwa kufungua mashauri manne (4) katika mahakama za Lindi na Liwale. Miongoni mwa mashauri yaliyofunguliwa mahakamani kwa kipindi cha robo ya tatu ni:

- Kufikishwa mahakamani watuhumiwa watatu kutokana na kujipatia fedha shilingi 92,562,449/= kwa njia za udanganyifu zilizotolewa kwa ajili ya fidia kupisha eneo la mradi wa kiwanda cha wanga, kesi hii ilisajiriwa na kupewa namba ECC 02/2021 inayowakabili Bw. Mohamed Mussa (Mpima ardhi) na wenzake wawili. Kesi bado inaendelea kusikilizwa katika mahakama ya wilaya ya Lindi

- Kufikishwa mahakamani watuhumiwa watano kutokana na kujipatia fedha sh 58,338,257 za wakulima wa zao la korosho katika chama cha ushirika cha msingi (Amcos) cha Umoja wilayani liwale, kesi hii ilisajiriwa na kupewa namba ECC 06/2021 inayowakabili Bw. Hamis Rahim Tewele (Katibu Umoja Amcos) na wenzake wanne kesi bado inaendelea kusikilizwa katika mahakama ya wilaya ya Liwale

Aidha hadi sasa jumla ya mashauri matano (5) yanaendelea kusikilizwa mahakamani na yapo katika hatua mbalimbali.

Ndugu wanahabari,

Katika kipindi hiki cha miezi mitatu (3) Januari 2021 hadi Machi 2021, TAKUKURU Mkoa wa Lindi kupitia Dawati la Kuzuia Rushwa ilifuatilia matumizi ya fedha za Miradi tisa ya Maendeleo yenye jumla ya thamani ya. Shilingi **977, 979,382.00** Kama ifuatavyo:

- Ujenzi wa vyumba vinne vya madarasa na Ofisi ya walimu, mabweni ya wavulana na wasichana Shule ya Sekondari KITOMANGA shilingi 250,000,000.00)
- Ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa, Ofisi ya walimu na Mashimo tano 5 ya vyoo Shule ya Msingi KIWALALA shilingi 45,500,000.00)
- Ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa, Ofisi ya walimu na Mashimo tano 5 ya vyoo Shule ya Msingi KILANGALA shilingi 45, 500,000.00)
- Ujenzi wa vyumba vinne vya madarasa, Ofisi ya walimu na Matundu tano ya vyoo Shule ya Sekondari KIWALALA shilingi 69,563,520.00) bila kuhusisha vifaa vilivyotolewa na Bebki ya NMB
- Mradi wa Maji kijiji cha NAMIKONGO- NACHINGWEA wenye thamani ya shillingi 315,374,112.00**.** Mradi huu umekamilika na unatumika.
- Mradi wa ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa na matundu nane (8) ya choo, shule ya msingi Michenga. 48,800,000/=
- Mradi wa ujenzi wa vymba viwili vya madarasa na matundu nane (7) ya choo, shule ya msingi Nangumbu shilingi 47,700,000/=
- Ufuatiliaji wa utekelezaji wa mfuko wa maenedeleo ya jamii awamu ya tatu (TASAF III) shilingi 125,541,750/=
- Ujenzi na ukarabati wa madarasa ya shule ya msingi Somanga EP4R shilingi 30,000,000/=

Baadhi ya Mradi iliyofuatiliwa imejengwa katika Ubora na mingine inaendelea kufanyiwa Ukaguzi wa ndani ili kubaini Thamani halisi ya fedha zilizotumika baada ya kuonekana kuwa na mapungufu. Mapungufu yote yaliyojitokeza katika baadhi ya miradi yalitolewa mapendekezo na kiasi cha fedha za miradi hii kilichokuwa kifanyiwe ubadhirifu kilidhibitiwa.

Ndugu wanahabari,

Katika kipindi cha Januari, 2021 hadi Machi, 2021 TAKUKURU Mkoa wa Lindi imeendelea kutekeleza malengo yake ya dawati la elimu kwa umma kwa kuwaelimisha wananchi wa

makundi mbalimbali na wadau wengine kuhusu rushwa na madhara yake kwa mtu mmoja mmoja, jamii, taasisi na taifa kwa ujumla.

TAKUKURU Mkoa wa Lindi imeendesha semina 13, imefanya mikutano ya hadhara 49. Pia TAKUKURU (M) Lindi imefanya ufunguzi na uimarishaji wa klabu za wanafunzi za wapinga rushwa 37, vipindi vya TV na Redio 3 na Utoaji wa makala au uandishi wa habari 6.

TAKUKURU INAYOTEMBEA:

Ndugu wanahabari

Katika kipindi cha januari hadi March, 2021 TAKUKURU kwa lengo la kusikiliza kero za wananchi ilikuja na mpango wa TAKUKURU inayotembea, TAKUKURU kwa kutekeleza mpango huu huamabatana na baadhi ya wakuu wa idara za Halmashauri ili kuweza kutatua karo za wananchi papo kwa papo na zile ambazo zinakuwa hazina majibu ya mara moja huchukuliwa na kufanyiwa kazi na majibu kutolewa. Katika mpango huu, wananchi wengi wamekuwa wakilalamikia matumizi mabaya ya madaraka ya viongozi katika maeneo ya kata na vijiji, ikiwemo kutopewa taarifa juu ya miradi ya maendeleo inayotekelezwa katika maeneo yao, kutosomwa kwa mapato na matumizi ya miradi inayosimamiwa na ngazi ya vijiji na kata. Hulalamikia pia migogoro ya ardhi isiyoisha, tozo mbalimabli za Halmashauri, kuchelewa kupata malipo ya mazao yao baada ya kuuzwa. TAKUKURU ikishirikiana na idara za Halmashauri na mamlaka zingine zimeweza kushughulikia malalamiko mbalimbali ynayoibuliwa kufuatia mapango huu wa TAKUKURU inayotembea. Baadadhi ya hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kuwaagiza viongoz ngazi ya vijiji na kata kubandika kwenye mbao za matangazo miradi inayotekelezwa, kusomwa kwa mapato na matumizi ya miradi inayosimamiwa katika maeneo ya vijiji na kata, Mkurugenzi kuyajengea uwezo mabaraza ya ardhi ya kata kupitia wanasheria wa Halamshauri ili mabaraza haya yaweze kufanya kazi zake kwa mujibu wa sheria.

Ndugu wanahabari,

Katika robo ya nne ya mwaka wa fedha 2020/2021 iliyoanza Aprili, 2021 TAKUKURU Mkoa wa Lindi umejipanga kuongeza juhudi katika ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi ya kimkakati iliopo Mkoani Lindi ikiwemo ya ujenzi wa miundombinu ya barabara, maji na miradi ya ujenzi

wa miundombinu wa madarasa ya shule za Msimgi na Sekondari, kukamilisha kuchambua mifumo ya ukusanyaji wa kodi na mapato ya serikali na kisha kuendesha warsha na wadau mbalimbali, na kuendelea kuelimisha umma madhara yaletwayo na vitendo vya rushwa. Pia Mkoa umejipanga kukamilisha chunguzi zinazotokana na taarifa mbalimbali zikiwemo taarifa za mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Ndugu wanahabari,

TAKUKURU Mkoa wa Lindi inaendelea kuwashukuru wananchi, vyombo vya Habari, pamoja na taasisi mbalimbali (binafsi na za serikali) katika Mkoa wa Lindi kwa ushirikiano mkubwa wanaoendelea kuutoa kwa ofisi zetu ikiwepo kutoa taarifa mbalimbali za vitendo vya rushwa. Aidha, tunawaomba wananchi na wadau wote waendelee kutuunga mkono kwa kutoa taarifa za vitendo vya rushwa kwa kutumia njia mbalimbali hususani kupitia simu yetu ya bure ya namba ya dharura **113** kwani mapambano dhidi ya rushwa si ya TAKUKURU peke yake bali ni ya jamii nzima kwa ujumla.

Imetolewa na:

Eng. Abnery J. Mganga

Mkuu wa TAKUKURU (M) Lindi